**OFISI YA RAIS, YAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA UKEREWE**

**SHULE YA SEKONDARI UKEREWE**




SHULE YA SEKONDARI UKEREWE

**S. L. P 198**

**NANSIO UKEREWE.**

**Mkuu wa shule: 0757 291 553.**

**M/mkuu wa shule (1) 0755 650 134, (2) 0753544864**


**MZAZI/MLEZI WA………………………………………………...**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI UKEREWE KWA MWAKA WA MASOMO WA 2024/2025.**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika shule hii kwa mwaka wa masomo 2024/2025 katika tahasusi ya CBG, HGL & HGLi
2. Mahali shule ilipo.
   Shule ipo umbali wa kilomita 12 kaskazini mwa mji wa Nansio ambao ni makao makuu ya halmashauri ya wilaya ya Ukerewe.
3. Muhula wa masomo unaanza tarehe .1/7/2024. Hivyo mwanafunzi anapaswa kuripoti tarehe hiyo na ndani ya siku 14 wanafunzi wote wanapaswa kuwa shuleni. Baada ya muda huo hakuna mwanafunzi wa chaguo la kwanza atakayepokelewa.
4. Muda wa kuripoti/kuwasili shuleni kuanzia saa **2:00 asubuhi** hadi **9:30 alasili** mwanafunzi atakayefika nje ya muda huo **hatapokelewa. “zinggatia muda uliotanjwa hapo juu”**

4. **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.**

   Michango ya shule

   Mchango wa uendeshaji wa shule Tsh 65,000/=

   Tahadhari Tsh 5,000/=

   Kitambulisho Tsh 5,000/=

   Nembo ya shule Tsh 5000/=

Jumla Tsh 80,000/=

**Malipo yote yafanyike kupitia benki ya CRDB A/C Na 0150651212000 yenye jina la UKEREWE SEKONDARY SCHOOL. Risiti za malipo ziwasilishwe siku ya kuripoti.**

Kwa wasio na bima ya afya waje na Tsh 5,000/= kwa ajili ya kukata bima ya CHF iliyoboreshwa kwa wakala wanaofanya kazi wilaya ya Ukerewe. Gharama ya matibabu nje ya bima ni jukumu la mzazi/mlezi.

a) Ikiwa mwanafunzi hataripoti ndani ya siku kumi na nne atakuwa amepoteza nafasi yake

C. Aje na:

I. Nakala ya (matokeo) result slip ya kidato cha nne

ii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.

iii. Fomu ya uchunguzi wa afya ya mwanafunzi iliyojazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali iwasilishwe siku ya kuripoti shuleni na kama kuna kiambata chochote juu ya afya ya mwanafunzi **tafadhali** njoo nacho.

D. Mzazi na mwanafunzi wanatakiwa kusoma na kujaza kwa makini na kusaini fomu ya sheria za shule. Mwanafunzi ahakikishe anakuja shuleni kusoma kwa bidii na si vinginevyo.

e) Nguo za nyumbani haziruhusiwi na asije nazo kabisa, mwanafunzi atavaa sare ya shule wakati wote awapo shuleni na wakati wa kuja kuripoti anatakiwa kuvaa sketi ya dark blue(iwe sentimetre 23 kutoka kwenye unyayo wa mguu) na shati nyeupe yenye mikono mirefu, shati isiwe na vashikizo vya chuma na sketi isiwe ya kubana. Mwanafunzi atakayekuja na nguo za kubana au fupi **hatapokelewa.**

f) Kila mzazi anawajibika kumpatia mwanae gharama za usafiri nyakati zote za likizo, pia gharama za matumizi yake binafsi. Hata hivyo unashauriwa kumpatia mwanafunzi fedha kwa kiasi Kwa ajili ya matumizi yake binafsi kwani kumpa fedha nyingi kunaweza kusababisha utovu wa nidhamu na kutozingatia masomo.

g) Mwanafunzi haruhusiwi kuja na vyakula shuleni.

h) Vyakula vinavyoruhusiwa ni; karanga za kusaga,bluuband na sukari pekee.

**5. SARE ZA SHULE**

a) Sketi mbili za darasani, kitambaa cha rangi nyeusi (sketi iwe ya rinda box, iwe na rinda kubwa mbele na nyuma, na marinda ya pembeni yawe mawili. Pia sketi iwe na mfuko). Unahimizwa kuhakikisha urefu wa sketi. (Sketi iwe sentimetre 23 kutoka kwenye unyayo wa mguu. Waislamu watavalia hijabu nyeupe yenye nembo pamoja na shati na skirt ya shule.NB juba zote ziendane na sale husika

b) Tshirt ya darasani pamoja na ile ya kushindia zinapatikana shuleni Kwa gharama ya TSH 12,000/= Kwa kila Moja (24,000 zote mbili).

c) Sketi mbili za dark blue (sketi ya malinda) zitakazovaliwa baada ya muda wa darasani.

d) Sweta moja rangi ya brown

e) Tai mbili na sketi mbili rangi nyeusi

f) Jezi nyekundu jozi moja na raba nyeupe za michezo jozi moja

g) Shati mbili nyeupe za mikono mirefu kitambaa cha tetron na ziwe na vishikizo vya kawaida na si vya chuma,

Soksi nyeupe jozi 4

i) Viatu vya kufunika vyeusi vya ngozi jozi mbili visivyo vya kuchongoka kwa mbele, viwe na visigino vifupi, vinavyong'arishwa kwa kiwi na kufungwa kwa Kamba.

j) Track suit kwa ajili ya kuvaa wakati wa maandalizi ya kujisomea usiku inapatikana shuleni Kwa gharama ya TSH 20,000/=

k) Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi na si kipala.

**6. MAHITAJI MENGINE**

a) Godoro la 3*2.5*6 na neti rangi ya blue ya kujikinga na mbu usiku.
b) Ream moja "double A" mbili kila mwaka unaruhusiwa kuzileta kwa awamu mbili ndani ya mwaka.
c) Shuka mbili rangi ya pink.
d) Mto wenye foronya ya pink.
e) Blanketi na nguo za kulalia
f) Taulo rangi nyeupe, ndala za kuogea, sandals, dawa ya meno, mswaki, sabuni za kutosha, kiwi, brashi, mafuta ya kujipaka.
g) Ndoo 2 za lita kumi, dishi moja na galoni moja ya lita 5 kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa, kijiko, sahani ya chuma, bakuli la chuma na kikombe cha nusu lita kwa ajili ya maji na uji.

Taa ya sola inayowaka vizuri na inayotunza umeme kwa muda mrefu kwa tahadhari ya umeme kukatika (ISIWE YA KUCHAJI KWA UMEME NA ISIWE NA SEHEMU ZINAZOWEZA KUCHAJI SIMU)

h) Madaftari makubwa 7 au Zaidi, Quire 4.
i) Scientific calculator kwa CBG/HGL
j) Dissecting kit kwa wanafunzi wa CBG na mkebe wa kalamu.
k) Sanduku la chuma kwa ajili ya kuhifadhia vitu na begi dogo la madaftari na vifaa vingine muhimu.

# Enga za kubandika pisi 4 Kwa ajili ya kuwekea neti bwenini.

**7. VIFAA VINGINE,**

a) hard broom moja, squeezer moja, jembe lenye mpini moja, fyekeo moja, moper moja na brashi ndogo ya chooni moja.

8. **MAAGIZO MUHIMU YA VITABU VYA KIADA NA ZIADA.**

Ili mwanafunzi aweze kuwa katika mazingira bora ya kujisomea anapaswa kuwa na vitabu. Orodha ya vitabu muhimu ni kama ifuatayo.

**LANGUAGE**

- The Real English Text Book For Advanced Level Foem 5 & 6 By KADEGHE MICHAEL, 2010
- Advanced English Language, Form 5 & 6 By DSM OXFORD UNIVERSITY PRESS, 2012.

- Advanced English Dictionary.

**GEOGRAPHY**

- General Geography in diagrams (R.E Bunnett)
- Practical Geography for Africa (John M Pritchard)
- Physical Geography for Africa. (D.T Msabila)
- Human and Economic Geography (D.T Msabila)

BIOLOGY

- Advanced Biology for secondary schools (Michael R)
- Biological science (Taylor O.J & Stoud G.W) • Cell Structure and Organization. (L. Msaki) • Understanding Biology- Fourth Edition.

**HISTORY**

- Mastering Advanced Level History book I and II (Kato – 2020)
- Basic Themes in European advanced level history paper I and II ( Ismail Ngobi 2021)
- Major Events in African History paper I (Fr Jovitus F. Kamara)
- Advanced Level history (form 5&6) OUP

**CHEMISTRY**

- Advanced level physical chemistry with general chemistry –APE networks 2012,1st edition 2011.
- Essential of physical chemistry-Arun Bahl
- Organic chemistry –Arun Bahl,1st edition illustrate Revised 2012.

**GENARAL STUDIES**

- General Studies for Advanced Level, Form five .Richard R. F Mbalase.
- General Studies, Supplementary Book for Advanced and Colleges, second edition-Konrad Adenaker

9**. VIAMBATANISHO MUHIMU.**

Kabla mwanafunzi hajafika shuleni ni lazima viambatisho vifuatavyo viwe vimejazwa.

a) Fomu ya uchunguzi wa afya (Medical Examination Form)
b) Fomu ya historia ya mwanafunzi na mikataba mbalimbali.
c) Nakala ya cheti cha Uraia/kuzaliwa kiwe na majina kamili kama yalivyo kwenye result slip. d) Nakala ya matokeo 'result slip.'

Tafadhali soma kwa umakini wa hali ya juu maelekezo haya na kuyatekeleza kwa ukamilifu wake kabla ya kuripoti shuleni kuja kuanza masomo.

HALMASHAURI YA WILAYA YA UKEREWE

SHULE YA SEKONDARI UKEREWE

SHERIA ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria na 10 ya mwaka 1995.

1. Ni kosa kwa mwanafunzi kuiba kitu chochote kile kikiwa ni cha mwenzake,mali ya shule au mali ya umma.
2. Ni kosa kwa mwanafunzi kuharibu kwa makusudi kitu cha mwenzake,mali ya shule au mali ya umma.
3. Ni kosa kwa mwanafunzi kutoka nje ya shule au kutohudhuria shule bila ruhusa
4. Ni kosa kwa mwanafunzi kugoma au kushiriki katika aina yoyote ile ya mgomo akiwa ndani au nje ya shule.
5. Ni kosa kwa mwanafunzi kutoheshimu picha za viongozi wa serikali, Bendera ya Taifa,Nembo ya Taifa,wimbo wa Taifa Fedha na maandishi ya serikali
6. Ni kosa kwa mwanafunzi kutosalimia, kutoheshimu au kutoonesha ukarimu kwa wakubwa wake katika kupokea mizigo kujituma kusaidia katika shughuli mbalimbali.
7. Ni kosa kwa mwanafunzi kutumia lugha chafu wakati wowote kwa mwanafunzi mwenzake,walimu,wafanyakazi na kwa watu wengine ndani na nje ya shule
8. Ni kosa kwa mwanafunzi kutoitikia Wito au kuchelewa mahali popote anapohitajika wakati wowote
9. Ni kosa kutohudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa
10. Ni kosa kutumia madawa ya kulevya, kunywa pombe,kuvuta bangi, sigara au aina yoyote ile ya tumbaku I l . Ni kosa kutembelea nyumba za walimu na wafanyakazi, vilabu vya pombe, kumbi za dansi(Mazinduke) na Video, nyumba za kulala wageni bila kibali maalumu.
12. Ni kosa kufanya au kujihusisha na vitendo vya uasherati,ushoga, ngono,kuoa au kuolewa
13. Ni kosa kutovaa sare ya shule inayokubalika wakati awapo shuleni au katika shughuli za kishule, kuonekana mchafu kwa kufuga nywele,ndevu,kucha,kunyoa kipara,kiduku,denge,kuvaa hereni,bangili,kofia,culture,viatu vya ghorofa na koti,kupaka kucha rangi na mapambo ya aina yoyote
14. Ni kosa kutosema ukweli au kutotoa ushahidi wa kweli unapohitajika kufanya hivyo
15. Ni kosa kuchafua mazingira kwa makusudi kwa kujisaidia ovyo,kukatisha viwanja na viunga vya shule,kukata miti, kutupa taka ovyo, kutofanya usafi katika maeneo uliyopangiwa na Viongozi wako na kupita karatasi au taka yoyote na usiiokote na kuitupa kwenye shimo la taka.
16. Kila mwanafunzi lazima ahudhurie shule kwa siku 194 kwa mwaka
17. Ni kosa mwanfunzi kufanya mawasiliano yoyote na wazazi au ndugu bila kupitia kwa uongozi wa shule. Mawasiliano yote yatafanyika kupitia uongozi wa shule kwa kuwa

    **MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUMILIKI SIMU YA MKONONI.**
18. Lugha ya mawasiliano ni Kiingereza. Kila mwanafunzi ajitahidi kujifunza kwa bidii na kujizoesha kuongea Kiingereza
19. Mgeni atakaye kutembelea sharti apate kibali kutoka Uongozi wa Shule. Ni marufuku kumtembeza mgeni yeyote katika maeneo ya Shule bila kibali cha Uongozi wa Shule.

NB: MAKOSA AMBAYO MWANAFUNZI AKIFANYA ANAFUKUZWA SHULE MOJA KWA MOJA

l. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi wa aina yoyote ile na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi,cocaine,mirungi,kubeli na kadhalika.
5. Makosa ya jinai
6. Kupigana au kupiga
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
8. Kudharau Bendera ya Taifa
9. Kuoa au kuolewa
10. Kupata mimba (wasichana)
I 1. Kuharibu au kutoa mimba (wasichana) ndani na nje ya shule
12. Kugoma,kuchochea,kuongoza au kuvuruga amani,usalama na Utulivu wa shule au watu
13. Kukataa/kugomea adhabu kwa makusudi
14. Kumiliki simu ya mkononi.

UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI KUKUBALIANA NA SHERIA ZA SHULE

Mimi.................................................................................................................................... (Jina la mwanafunzi)

tahasusi... ...... ...... ... .... .. . ...Nakubaliana na sheria zote za shule naahidi kwamba kwa muda wote nitakaokuwa mwanafunzi wa shule ya Sekondari Ukerewe nitatii, kufuata na kutekeleza sheria na taratibu zote za shule kwa moyo wa dhati.Nitakuwa tayari kuadhibiwa iwapo kufuata au nitavunja sharia hizo.

JINA LA MWANAFUNZI...................... ......…………..SAHIHI. .. . .. . .. . . . …………JINA LA MZAZI/MLEZI……………………...................…… SAHIHI…………………………

SAHIHI YA MKUU WA SHULE…………………… MUHURI...............................

TAREHE………………………….

MKATABA WA KUTOSHIRIKI MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

Mimi (Jina la mwanafunzi)....…………..…………………………………………..……… . ...wa kitongoji cha...................................kijiji cha.. . . . . .................... ...kata ya. ...................…............... Tarafa ya

………………………….....wilaya ya..…………………….…..Mkoa wa…………….. . . .. . . . ....naahidi mbele ya wazazi/walezi wangu ambao ni

Jina…………………………………...uhusiano................................

Jina……………………………………..uhusiano…………………………..

kuwa kwa kipindi chote nitakachokuwa Shule ya Sekondari Ukerewe nikiwa mwanafunzi kwa njia yoyote ile sitoanzisha wala kushiriki katika migomo/fujo wala kujihusisha kutenda makosa ya jinai kwa kisingizio chochote kile kwa kutambua kuwa makosa hayo hulisababishia Taifa hasara kubwa hivyo nitakuwa mstari wa mbele kudumisha amani shuleni hivyo nitapoona haki haitendeki nitatumia taratibu zilizowekwa ili haki itendeke na si vinginevyo..

Endapo nitakiuka ahadi hii natambua kuwa nitakuwa nimetenda kosa na nitastahili kufukuzwa shule kwa kutenda kosa kwa kukusudia

JINA LA MWANAFUNZI………………………………… SAHIHI…………………….

JINA LA MZAZI/MLEZI……………………………………SAHIHI…………………….

SAHIHI YA MKUU WA SHULE……………………………….MHURI………………….

TAREHE………………………………

MKATABA WA KULIPA KARO, MICHANGO NA MAHITAJI MENGINE KWA WAKATI

. Mimi..........................................................................ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi.......................................tahasusi.. ………………….. .ambaye ni (uhusiano)............................nakiri kukubaliana na sheria,kanuni na taratibu za kulipa ada, michango na mahitaji mengine ya shule kama yalivyotolewa na Shule na kwamba natambua kuwa mwanangu anatakiwa kuhudhuria shule jumla ya siku 194 bila kukosa na pale atakapokuwa na tatizo nitaleta taarifa shuleni mara moja bila kuchelewa. Pia nitafuatailia maendeleo yake kitaaluma mara kwa mara.(**Mwanafunzi atakaycghushi saini ya mzazi/mlezi ataadhibiwa ikiwezekana atafukuzwa Shule moja kwa moja, hivyo mzazi/mlezi aweke saini yake mwenyewe badala ya saini kuwekwa na mwanafunzi ili kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza baadaye)**

Jina la mzazi/mlezi . . . ………………………………saini. ………………………

Simu……………………………………. Tarehe…………………………..

**SHULE YA SEKONDARI UKEREWE**

**S.L.P 41 NANSIO - UKEREWE**

Shule ya sekondari ukerewe haina utaratibu wa kuwatembelea wanafunzi kama kuna changamoto yoyote kwa mwanafunzi mzazi/mlezi utajulishwa haraka kwa njia ya simu na endapo kama kuna ulazima wa mzazi/mlezi kufika shule utakuja kwa wito maalum. Mzazi/ mlezi Pamoja na ndugu wa karibu weka picha na namba za simu katika jedwali lifuatalo kwa ajili ya mawasiliano Zaidi

| NA | TAARIFA | 1 | 2 |
|---|---|---|---|
| 1 | Jina la ndugu | | |
| 2 | Kazi yake | | |
| 3 | Uhusiano naye | | |
| 4 | Anakoishi | | |
| 5 | Anuani yake | | |

| | | |
|---|---|---|
| | Simu yake (Ya mkononi) | |
| | | Picha ya Rangi (Pasport size) |

NB: a. Hawa waorodheshwe na mzazi/mlezi mwenyewe na si mwanafunzi
b. hii hapa chini ndiyo jezi ya michezo hakikisha bukuta yake ni ndefu

UKEREWE SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 41 NANSIO-UKEREWE
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

TO THE MEDICAL OFFICER

________________________________________

________________________________________

________________________________________

(To be completed by Government Medical officer)

Student's full name………………………………………………………………..

Age (Years)..........................................................................................................

Please Examine the named student as to his physical and mental fitness for enrollment as an A-Level student. The examination should include the following:

Blood count (red and white).....

Stool examination..........................................................................................................

Urine analysis... ................................................ ………………………………………

Syphilis and other venereal diseases test..................................................................................

T.B ……………………………………………………………………………………..

Eye sight..............................................................................................................................

Ears ……………………………………………………………………………………..

Chest Examination.................................................................................................... .. .

Spleen ……………………………………………………………………………………..

Leprosy..............................................................................................................................

Neuroses............................................................................................................................

Abdomen ………………………………………………………………………………………

Urine for plant test................................................................................................................

Speech..................................................................................................................................

Limbs......... .... ....................................................................................................................

Epilepsy................................ ……………………………………………………………….. ANY ADDITIONAL INFORMATION AND RECOMMENDATIONS e.g. Physical defect, chronic or Family diseases etc

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

I certify that the person named above is fit/unfit to pursue further studies in advanced level

Station ………………………………………………………………………………………..

Name……………………………………………………………………………………….

Signature ...........................................................................................................................

Date....................................................

Official stamp